# BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

## TAARIFA YA MATOKEO YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI (PSLE) SEPTEMBA, 2018

**Imetolewa na :**

**KATIBU MTENDAJI**
**23 OKTOBA, 2018**

# TAARIFA YA MATOKEO YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI (PSLE) SEPTEMBA, 2018

## 1.0 UTANGULIZI

Katika Mkutano wake wa **126** uliofanyika tarehe **22/10/2018**, Baraza la Mitihani la Tanzania liliidhinisha kutangazwa kwa matokeo ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi ulifanyika kuanzia tarehe **05** hadi **06 Septemba, 2018**.

## 2.0 USAJILI WA WATAHINIWA

Jumla watahiniwa **957,904** wa Shule za Msingi walisajiliwa kufanya mtihani huo wakiwemo wasichana **502,790** sawa na asilimia **52.49** na wavulana **455,114** sawa na asilimia **47.51**. Kati ya watahiniwa waliosajiliwa, watahiniwa wenye mahitaji maalum walikuwa **2,820** sawa na asilimia **0.29**.

Watahiniwa **944,218** sawa na asilimia **98.57** ya waliosajiliwa walifanya mtihani. Kati yao wasichana walikuwa **496,857** sawa na asilimia **98.82** na wavulana walikuwa **447,361** sawa na asilimia **98.30**. Watahiniwa **13,686** sawa na asilimia **1.43** hawakufanya mtihani kutokana na sababu mbalimbali, zikiwemo utoro na ugonjwa. Kati yao wasichana ni **5,933** na wavulana ni **7,753**.

## 3.0 MATOKEO YA WATAHINIWA

### 3.1 Ufaulu wa ujumla

Jumla ya watahiniwa **733,103** kati ya **943,318** (wasichana **496,427** na wavulana **446,891**) waliotunukiwa matokeo wamefaulu. Watahiniwa hawa wamepata alama **100** au zaidi kati ya alama **250**. Idadi hii ya watahiniwa waliofaulu ni sawa na asilimia **77.72**. Kati yao wasichana ni **382,830** ambao ni sawa na asilimia **77.12** na wavulana ni **350,273** sawa na asilimia **78.38**. Mwaka **2017** watahiniwa waliofaulu walikuwa asilimia **72.76**, hivyo kuna ongezeko la ufaulu kwa asilimia **4.96**.

Mchanganuo wa ufaulu katika madaraja mbalimbali umeainishwa katika Jedwali lifuatalo:

| Daraja | Wavulana | | Wasichana | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia |
| A | 27,559 | 6.17 | 19,781 | 3.98 | 47,340 | 5.02 |
| B | 145,075 | 32.46 | 136,166 | 27.43 | 281,241 | 29.81 |
| C | 177,639 | 39.75 | 226,883 | 45.70 | 404,522 | 42.88 |
| **A-C** | **350,273** | **78.38** | **382,830** | **77.12** | **733,103** | **77.72** |
| D | 77,018 | 17.23 | 97,589 | 19.66 | 174,607 | 18.51 |
| E | 19,600 | 4.39 | 16,008 | 3.22 | 35,608 | 3.77 |

## 3.2 Ufaulu Kimasomo

Takwimu za matokeo zinaonesha kuwa ufaulu katika masomo ya **English Language**, **Maarifa ya Jamii**, **Hisabati**, na **Sayansi** umepanda kwa asilimia kati ya **4.03** na **11.92** ikilinganishwa na mwaka 2017. Aidha somo la **Kiswahili**, ufaulu wake umeshuka kidogo kwa asilimia **1.44** ikilinganishwa na mwaka 2017. Watahiniwa wamefaulu zaidi katika somo la **Kiswahili** ambapo ufaulu ni asilimia **85.42** na somo walilofaulu kwa kiwango cha chini zaidi ni **English Language** lenye ufaulu wa asilimia **49.63**. Mchanganuo zaidi katika ufaulu wa masomo umeainishwa katika Jedwali lifuatalo:

| SOMO | MWAKA | WENYE MATOKEO | WALIOFAULU (GREDI A-C) | | WENYE GREDI D | | WENYE GREDI E | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| KISWAHILI | 2017 | 909,884 | 790,294 | 86.86 | 89,192 | 9.80 | 30,398 | 3.34 |
| | **2018** | **943,211** | **805,685** | **85.42** | **95,950** | **10.17** | **41,576** | **4.41** |
| ENGLISH | 2017 | 909,817 | 366,656 | 40.30 | 444,444 | 48.85 | 98,717 | 10.85 |
| | **2018** | **943,256** | **468,092** | **49.63** | **367,636** | **38.98** | **107,528** | **11.40** |
| MAARIFA YA JAMII | 2017 | 909,877 | 570,782 | 62.73 | 284,973 | 31.32 | 54,122 | 5.95 |
| | **2018** | **943,260** | **694,472** | **73.62** | **198,051** | **21.00** | **50,737** | **5.38** |
| HISABATI | 2017 | 909,865 | 492,259 | 54.10 | 295,359 | 32.46 | 122,247 | 13.44 |
| | **2018** | **943,252** | **622,718** | **66.02** | **226,901** | **24.06** | **93,633** | **9.93** |
| SAYANSI | 2017 | 909,872 | 660,642 | 72.61 | 209,595 | 23.04 | 39,635 | 4.36 |
| | **2018** | **943,246** | **722,885** | **76.64** | **170,823** | **18.11** | **49,538** | **5.25** |

## 4.0 WATAHINIWA BORA KITAIFA

Watahiniwa bora kitaifa ni wale ambao wamepata alama nyingi zaidi kuliko wenzao kwenye masomo matano waliyotahiniwa na wameoneshwa kama ifuatavyo:

**a) Watahiniwa kumi (10) bora kitaifa**

| NA. | JINA | JINSI | SHULE | MKOA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | NDEMEZO RUTAKWA LUBONANKEBE | M | KADAMA | GEITA |
| 2. | INNOCENT PAUL SELELI | M | CARMEL | MOROGORO |
| 3. | GIVEN COSMAS MALYANGO | F | TUMAINI JUNIOR | ARUSHA |
| 4. | DIOMEDES JAMES MBOGO | M | ST. ACHILEUS KIWANUKA | KAGERA |
| 5. | SWEETBERT JOSEPH JOHN | M | MINGAS | SHINYANGA |
| 6. | NAJMA MUNA MANJI | F | NYAMUGE | MWANZA |
| 7. | BEATRICE BARAKA JEREMIAH | F | MAPINDUZI B | MARA |
| 8. | MOHAMED ABDIRAHMAN MOHAMED | M | RASKAZONE | TANGA |
| 9. | LUQMAN SULTAN ALLY | M | RASKAZONE | TANGA |
| 10. | FRANCISCO ALPHONCE MAIGA | M | KADAMA | GEITA |

**b) Wasichana kumi (10) bora kitaifa**

| NA. | JINA | SHULE | MKOA |
|---|---|---|---|
| 1. | GIVEN COSMAS MALYANGO | TUMAINI JUNIOR | ARUSHA |
| 2. | NAJMA MUNA MANJI | NYAMUGE | MWANZA |
| 3. | BEATRICE BARAKA JEREMIAH | MAPINDUZI B | MARA |
| 4. | HAMISA ALLY KASELE | TUSIIME | DAR ES SALAAM |
| 5. | KAREEN CHARLES GABRIEL | TUSIIME | DAR ES SALAAM |
| 6. | ROSE COSMAS SAMSON | NYAMUGE | MWANZA |
| 7. | RAHMA JUMA SHAABAN | FOUNTAIN GATE | DAR ES SALAAM |
| 8. | ASHURA WILLY MEMBA | HAVARD | DAR ES SALAAM |
| 9. | CAREEN EMANUEL PALLANGYO | MARTIN LUTHER | DODOMA |
| 10. | MERLYN GODSON MOLLEL | GREEN ACRES | ARUSHA |

c) **Wavulana kumi (10) bora kitaifa**

| NA. | JINA | SHULE | MKOA |
|---|---|---|---|
| 1. | NDEMEZO RUTAKWA LUBONANKEBE | KADAMA | GEITA |
| 2. | INNOCENT PAUL SELELI | CARMEL | MOROGORO |
| 3. | DIOMEDES JAMES MBOGO | ST. ACHILEUS KIWANUKA | KAGERA |
| 4. | SWEETBERT JOSEPH JOHN | MINGAS | SHINYANGA |
| 5. | MOHAMED ABDIRAHMAN MOHAMED | RASKAZONE | TANGA |
| 6. | LUQMAN SULTAN ALLY | RASKAZONE | TANGA |
| 7. | FRANCISCO ALPHONCE MAIGA | KADAMA | GEITA |
| 8. | MASOUD SALEHE KITOBOLI | ZUGIMLOLE | TABORA |
| 9. | AMON HAGAI JARED | TUSIIME | DAR ES SALAAM |
| 10. | ELIAH EXAVERY INONGU | MZIGU | MWANZA |

## 5.0 MPANGILIO WA SHULE KWA UBORA WA UFAULU

Shule zenye idadi ya watahiniwa zaidi ya 40 zimepangwa kwa ubora wa ufaulu kama ifuatavyo:

a) **Shule 10 bora Kitaifa**

| NAMBA | JINA LA SHULE | IDADI | MKOA | NAFASI |
|---|---|---|---|---|
| PS2007031 | RASKAZONE | 55 | TANGA | 1 |
| PS1301069 | NYAMUGE | 114 | MWANZA | 2 |
| PS0904095 | TWIBHOKI | 71 | MARA | 3 |
| PS1701035 | KWEMA MODERN | 45 | SHINYANGA | 4 |
| PS1701064 | ROCKEN HILL | 50 | SHINYANGA | 5 |
| PS0204115 | ST. ANNE MARIE | 59 | DAR ES SALAAM | 6 |
| PS0508024 | JKIBIRA | 70 | KAGERA | 7 |
| PS0505183 | ST. ACHILEUS KIWANUKA | 76 | KAGERA | 8 |
| PS0501076 | ST SEVERINE | 65 | KAGERA | 9 |
| PS0502139 | RWEIKIZA | 120 | KAGERA | 10 |

b) **Shule 10 ambazo hazikufanya vizuri**

| NAMBA | JINA LA SHULE | IDADI | MKOA | NAFASI |
|---|---|---|---|---|
| PS2003083 | MANGIKA | 62 | TANGA | 1 |
| PS1901078 | MWAZIZI | 42 | TABORA | 2 |
| PS2706020 | ISEBANDA | 56 | SIMIYU | 3 |
| PS1901047 | MALAGANO | 52 | TABORA | 4 |
| PS0907043 | MAGANA | 84 | MARA | 5 |
| PS1106041 | KODODO | 69 | MOROGORO | 6 |
| PS2003124 | MTINDILI | 92 | TANGA | 7 |
| PS1606035 | LUMALU | 41 | RUVUMA | 8 |
| PS0301012 | CHIDETE | 37 | DODOMA | 9 |
| PS2003087 | MAVULUI | 93 | TANGA | 10 |

## 6.0 MPANGILIO WA MIKOA NA HALMASHAURI/MANISPAA/JIJI KIUFAULU

(a) **Mikoa 10 iliyoongoza Kitaifa**

| MKOA | IDADI | WALIOFAULU (A-C) | ASILIMIA | NAFASI |
|---|---|---|---|---|
| DAR ES SALAAM | 70,303 | 64,861 | 92.26 | 1 |
| GEITA | 37,347 | 33,062 | 88.53 | 2 |
| ARUSHA | 37,840 | 33,035 | 87.3 | 3 |
| KILIMANJARO | 36,749 | 31,534 | 85.81 | 4 |
| KAGERA | 46,842 | 39,545 | 84.42 | 5 |
| MWANZA | 65,896 | 55,330 | 83.97 | 6 |
| IRINGA | 25,621 | 21,325 | 83.23 | 7 |
| MTWARA | 24,459 | 20,100 | 82.18 | 8 |
| KATAVI | 9,868 | 7,967 | 80.74 | 9 |
| NJOMBE | 19,326 | 15,507 | 80.24 | 10 |

(b) **Halmashauri 10 zilizoongoza Kitaifa**

| HALMASHAURI / MANISPAA | MKOA | IDADI | WALIOFAULU (A-C) | ASILIMIA | NAFASI |
|---|---|---|---|---|---|
| ARUSHA(M) | ARUSHA | 10,630 | 10,357 | 97.43 | 1 |
| MOSHI(M) | KILIMANJARO | 3,455 | 3,324 | 96.21 | 2 |
| KINONDONI | DAR ES SALAAM | 12,477 | 11,940 | 95.70 | 3 |
| ILALA(M) | DAR ES SALAAM | 13,068 | 12,492 | 95.59 | 4 |
| CHATO | GEITA | 6,503 | 6,180 | 95.03 | 5 |
| ILEMELA | MWANZA | 8882 | 8420 | 94.80 | 6 |
| MAFINGA MJI | IRINGA | 1,822 | 1,692 | 92.86 | 7 |
| HAI | KILIMANJARO | 4,575 | 4,237 | 92.61 | 8 |
| MWANZA JIJI | MWANZA | 10,319 | 9,524 | 92.30 | 9 |
| KIGAMBONI | DAR ES SALAAM | 3,448 | 3,180 | 92.23 | 10 |

## 7.0 MATOKEO YA MTIHANI YALIYOZUILIWA

Baraza la Mitihani la Tanzania limezuia kutoa matokeo ya Watahiniwa **120** ambao waliugua/walipata matatizo na kushindwa kufanya mtihani kwa masomo yote au baadhi ya masomo. Watahiniwa husika wamepewa fursa nyingine ya kufanya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE) 2019 kwa mujibu wa kifungu **32** (**1**) cha Kanuni za Mitihani.

## 8.0 MATOKEO YA MTIHANI YALIYOFUTWA

Baraza la Mitihani la Tanzania limeyafuta matokeo yote ya watahiniwa **357** waliobainika kufanya udanganyifu katika Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi (**PSLE**) **2018** kwa mujibu wa kifungu **30**(**2**)(**b**) cha Kanuni za Mitihani. Aidha, Baraza limezishauri mamlaka zinazohusika kuwachukulia hatua wale wote waliohusika kwa namna moja au nyingine kusababisha kutokea kwa udanganyifu wa mitihani kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi na Sheria za Nchi yetu.

## 9.0 TATHMINI YA AWALI YA MATOKEO

Matokeo ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi (**PSLE**) **2018** yanaonesha kuwa ufaulu wa jumla umepanda kwa asilimia **4.96** ukilinganishwa na mwaka **2017**. Aidha, ufaulu wa watahiniwa katika masomo ya **Kiswahili**, **Sayansi**, **Maarifa ya Jamii** na **Hisabati** uko juu ya wastani. Hata hivyo, takwimu za matokeo zinaonesha kuwa ufaulu katika somo la **Kiingereza** uko chini ya wastani japokuwa unaendelea kuimarika mwaka hadi mwaka. Hivyo, juhudi za makusudi zinahitajika kuendelea kufanyika ili kuinua kiwango cha ufaulu wa somo hili.

Baraza la Mitihani litafanya uchambuzi wa kina wa matokeo haya kwa kila somo na kutoa machapisho ya uchambuzi huo yatakayowasilishwa kwa wadau wa elimu, zikiwemo shule zote za msingi nchini kwa lengo la kuwawezesha walimu kutumia taarifa za uchambuzi katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji shuleni.

## 10.0 PONGEZI ZA BARAZA

Baraza la Mitihani la Tanzania linapenda kutumia fursa hii kuzipongeza Kamati za Uendeshaji Mitihani za Mikoa na Manispaa/Halmashauri nchini kwa kazi nzuri waliyoifaya ya kusimamia kwa umakini taratibu zote za uendeshaji wa mitihani ya Taifa.

Baraza linawapongeza wanafunzi wote waliofanya vizuri katika mtihani wao wa Kumaliza Elimu ya Msingi (**PSLE**) **2018** na kuwataka waendelee kufanya bidii katika kujifunza ili kuimarika zaidi kitaaluma watakapoendelea na ngazi ya elimu ya sekondari.

## 11.0 HITIMISHO

Ili kuwezesha wanafunzi na wadau wa elimu kuona matokeo haya kwa urahisi, Baraza limeyaweka matokeo hayo kwenye **TOVUTI** zifuatazo: www.necta.go.tz, www.moe.go.tz, www.poralg.go.tz na www.tanzania.go.tz.

Baraza la Mitihani la Tanzania limewasilisha Matokeo hayo kwenye Mamlaka zinazohusika ili zifanye uchaguzi wa watahiniwa wa kujiunga na elimu ya Sekondari. Hivyo, matokeo ya uchaguzi wa watahiniwa kujiunga na Kidato cha Kwanza yatatangazwa na Mamlaka husika mara baada ya zoezi la uchaguzi kukamilika.

Dkt. Charles E. Msonde
**KATIBU MTENDAJI**
**23/10/2018**